
HAYATI HASSAN MWALIMU MBEGA

M.M. Mulokozi

Mshairi, Marehemu Hassan Mwalimu Mbega (1914 – 2007) alizaliwa Jego, Vanga, katika wilaya ya Kwale nchini Kenya. Baba yake, Mwalimu bin Mbega, vilevile alikuwa mshairi na mwimbaji. Mama yake, Mwunguja bint Mwakombo, alikuwa mtu wa Tongoni, Tanga. Hassan Mbega alisomea Tanga kati ya mwaka 1922-28. Mwaka 1928-1932 alifanya kazi ya useremala mjini Tanga. Kuanzia mwaka 1935 hadi 1989 alikuwa mwalimu wa Kiswahili mjini Mombasa, na baadaye Nairobi. Mshairi ameacha nyuma watoto 10 na wajukuu kadha.

Mwalimu Mbega alikuwa mwanazuoni mwenye upeo mkubwa kuhusiana na taaluma ya Kiswahili na ushairi. Alianza kutunga mashairi kwenye miaka ya 1930. Mwalimu wake wa ushairi alikuwa ni Shariff Alawi bin Nassir wa Wasini. Mongoni mwa kazi zake zilizochapishwa ni hizi zifuatazo:

- Upisho wa Malenga
- Dafina ya Malenga
- Utenzi wa Mfalme Mwadilifu
- Wasia Bora na Hadithi Zake

Hayati Hassan Mbega alipata kutunukiwa tuzo ya ushairi na Chama cha Walimu wa Kiswahili cha Kenya.

[Mwandishi wa maelezo haya, M.M. Mulokozi, alibahatika kukutana na kufanya mahojiano na Mwalimu Hassan Mbega jijini Nairobi mwaka 1994. Kwa maelezo zaidi soma M.M. Mulokozi na T.S.Y.Sengo History of Kiswahili Poetry, TUKI, 1995: 62-63. Taarifa zaidi kuhusu hayati Mbega zinahitajika. Wenye taarifa wawasiliane na Mhariri, Mulika, S.L.P. 35110, TATAKI, Dar es Salaam; Barua pepe: ikr@udsm.ac.tz]

SHAIRI: MUNGU AMLAZE PEMA

*Alamin Siwa Somo
(Malenga wa Mombasa)*

Somo naipija mbiu, ipae bara na pwani.
Kwanzia Kismau, hadi (na) Malaba ndani.
Tumeingiwa na kiu, ilotukaba kooni.
Ile ya kumsahau, Mwalimu wetu Hassani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Ametupoka Ghafura, Illahi Mola Dayani.
Kwa mauti kumdara, hayu tena duniani.
Kwa hivi tutasorora, hakuwi kama zamani.
Kwa kupunguwa kung'ara, ni kwisha hapatikani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Hupatikana kwa tabu, vile vilo na thamani.
Mfano kama dhahabu, mpaka uchimbe chini.
Na vyengine vya ajabu, lulu hutoka shazani.
Vikitwacha ni adhabu, watu huwa majonzini.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Hassani Mbega Mwatsui, shujaa nambari wani.
Hivi hatujitambui, kwa ukiwa vifuani.
Nikimuomba sa hii, Illahi ya Rahamani.
Ampe yalo shufai, mazuri yaso kifani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Katutungia vitabu, vilo na thamani ndani.
Vya uzuri wa ajabu, twavisoma hatukani.
Hivi tu kama mabubu, kwani tutayatamani.
Maandishi ya dhahabu, tena hayapatikani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Na pia niyatamke, wasikie redioni.
Nawaomba tungo zake, wapeperushe angani.
Iwe ni ishara kwake, heshima kote nchini.
Ya kwamba itambulike, Shuja' kenda kaburini.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Rambi rambi nazituma, ziende hadi nyumbani.
Kwa familia nzima, yake ya Bwana Hassani.
Wasubiri kwa salama, subira iso kifani.
Kwani kufa ni lazima, sote tulo duniani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.

Mwisho hapa nikituwa, mtunzi mum'baini
Ni mimi mwana wa Siwa, jina langu Alamini.
Nilojawa na ukiwa, na jakamoyo moyoni.
Mikono nikiinuwa, na kumuomba Manani.
Mungu amlaze pema, pa watu wema peponi.